


## **JINSI YA KUMTAMBUA NG'OMBE ALIYE KWENYE JOTO**

Ng'ombe (jike) kuwa kwenye joto ni kipindi kile ambacho ng'ombe jike au mtamba anakubali kupandwa na dume dalili inayoonyesha kuwa yali lipo tayari kutolewa kutoka kwenye ovari kwa ajili ya kurutubishwa na mbegu ya ng'ombe dume. Kwa kawaida ng'ombe jike aliyebarehe huingia kwenye joto kila baada ya siku 18-24 kama hajashika mimba na wastani ni siku 21. Heifer anafaa apandishwe akifikisha umri wa miezi kati ya 14-18. Na ng'ombe hurudi kwenye joto baada ya siku 38 na 42 tangu azae, lakini muda unaoshauriwa kupandishwa tena ni kati ya miezi 2-3 tangu azae. Ng'ombe hubeba mimba kwa muda wa miezi 9 na nusu na inafaa azae ndama mmoja kwa mwaka.

Utambuzi wa joto kwenye ng'ombe ni wa muhimu sana hasa wafugaji wanao pandisha ng'ombe kwa njia ya chupa (Artificial insemination), wanatumia mfumo wa kuhamishia vitoto kwa majike (Embryo transfer) na wale wanaochanganya madume na majike wakati wa kupanda tu. Mara nyingi ng'ombe wa kienyeji hawahitaji uangalizi huu kama ng'ombe majike na madume wamechanganyikana, lakini kama mfugaji hana madume na anategemea kwa jirani basin aye itabidi atumie dalili kumtambua ng'ombe aliye kwenye joto. Japo njia ya kutumia madume yaliyoko kwenye shamba hayo muda wote si njia nzuri kwani inaweza kusababisha muendelezo wa magonjwa na hata kupunguza ubora wa ng'ombe. Kwa wafugaji wa kienyeji ni vema wakajenga mfumo wa kubadlishana madume ili uepuka athari zilizotajwa hapo juu. Kama unatumia mfumo wa madume izingatiwe kuwa dume mmoja inashauriwa apande majike 20 hadi 25 tu ili uzalishaji uwe bora.

## **DALILI ZA NGOMBE MWENYE JOTO**

Ni muhimu kufahamu ni dalili ipi ya kuu wakati unaangalia mabadiliko ya ng'ombe wako itakayo kusaidia kumpandisha ng'ombe wako. Ipo dalili kuu ya msingi moja inayoashiria sasa ng'ombe anatakiwa kupandwa na dume au kupandishwa ambayo ni **"ng'ombe kusimama ili apandwe na wengine"** (dalili sahihi ya joto). Hii dalili ipo katika kundi dalili linaloitwa *ng'ombe kuwa kwenye joto* ambalo lipo kati ya kundi *la ng'ombe kuja kwenye joto* na *ng'ombe kutoka kwenye joto* kama zilivyoielezwa hapa chini. Na dalili hizi zinaweza kuchukua muda wa masaa 30



**a) Dalili za ngombe kuingia kwenye joto (Masaa 8)**

Hizi ni dalili zinazojitokeza mapema zikiashiria kuingia kwenye joto kamili ambazo ni:

- Ng'ombe kusimama na kuunguruma
- Kuzunguka zunguka (mtukutu)
- Kuwanusa na kuwaramba majike wenzake sehemu ya nje ya uzazi/uke
- Kuinua kichwa na kupindisha midomo mara baada ya kunusa hasa ikigundulika kuwa ng'ombe yuko kwenye joto.
- Kuwapiga kikumbo kwa kichwa wenzake

-Atajaribu kuwapanda majike wenzake lakini hata simama kupandwa

-Sehemu ya nje ya kizazi/uke (vulva) huwa nyekundu, imevimba (umuka) na yenye unyevunyevu

-Kutoka ute angavu sehemu ya nje ya uzazi/uke (vulva)

### **b) Dalili za ng'ombe kuwa kwenye joto (Masaa 18)**

Ng'ombe **kusimama ili apandwe** ndiyo dalili sahihi ya ng'ombe kuwa kwenye joto, ng'ombe anaweza kutembea kidogo kwasababu ya kusukumwa na uzito wa ng'ombe anayempanda.



Dalili nyingine ni kama ifuatavyo:

-Kuwapanda ng'ombe wengine

- Kuinua kichwa na kupindisha midomo mara kwa mara baada ya kunusa na kugundulika kuwa ng'ombe yuko kwenye joto na hukojoa mara kwa mara.

-Kuunguruma mara kwa mara

-Kuwa mtukutu na mwoga

-Kupumzisha kidevu na kupangusa juu ya kiuno (mwanzoni mwa mkia) cha jike mwenzake, hapa ng'ombe wote waangaliwe kwa dalili kuu maana wote wanaweza kuwa kwenye joto.

-Kupungua kwa utoaji maziwa na ulaji wa chakula



**c) Dalili za ng'ombe anayetoka kwenye joto (zaidi ya masaa 14)**

-Atajaribu kuwapanda majike wenzake lakini hata simama kupandwa

-Kuwanusa na kuwaramba majike wenzake sehemu ya nje ya uzazi/uke

-Kutoka ute angavu sehemu ya nje ya uzazi/uke (vulva)

-Baadhi ya majike na mitamba wengi hutoa damu siku mo au tatu mara baada ya kutoka kwenye joto. Dalili hii ni ishara kuwa ng'ombe huyo alikuwa kwenye joto na haina maana kuwa ng'ombe ameshindwa kushika mimba. Hata hivyo ng'ombe hawa watazamwe kama watarudi kwenye joto siku ya 18 au 19.